

Je, gongo na sigara husaidia uyeyushaji wa chakula?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ni imani na fikra potofu kwamba, ukinywa gongo au kuvuta sigara kwa kiasi kidogo baada ya chakula itasaidia kuyeyusha baadhi ya vyakula vya mafuta. Pombe inaweza hata kupunguza mtiririko wa kawaida wa kimiminika muhimu kwa uyeyushaji wa chakula (tindikali) na hivyo kuchelewesha kuliko kurahisisha uyeyushaji wa chakula. Nikotini ya sigara kwa upande mwingine inaongeza kazi katika utumbo mpana na hivyo kurahisisha uyeyushaji wa chakula. Lakini kwa upande mwingine nikotini huchochea utengenezaji wa tindikali tumboni ambayo husababisha maumivu ya tumbo.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25327>